

HAKI ZA BINADAMU

Na Wakili Manace Ndoroma

Haki za Binadamu ni nini?

Hizi ni haki ambazo mtu anazipata mara tu anapozaliwa, na anaendelea kuwa nazo hadi kifo chake. Kwa maneno mengine, kitendo cha kuzaliwa ukiwa mwanadamu na si kiumbe kingine kinakupa moja kwa moja haki fulanifulani ambazo viumbe vingine havina. Kwa hiyo, haki za binadamu zipo tu, hata kama hazijaandikwa popote, tofauti na haki za kisheria ambazo huanza pale sheria husika inapotungwa, na hufika tamati pale ambapo sheria husika imefutwa.

Mifano michache ya haki za binadamu ni pamoja na haki ya kuishi, haki ya kuwa na makazi, haki ya kutoadhibiwa bila kusikilizwa, haki ya mtu kwenda anakotaka, haki ya kutodhalilishwa na kutwezwa kwa utu, haki ya kumiliki mali, nk.

Kutokana na umuhimu wake, katika nchi mbalimbali haki za binadamu zimewekewa mifumo maalum ya kuzilinda na kuhakikisha hazivunjwi hovyovhovy. Katika nchi ya Tanzania kwa mfano, ipo Tume ya Haki za Binadamu na Utwala Bora ambayo iliundwa mwaka 2001 kwa ajili ya kuhakikisha kwamba kila mtu, awe kiongozi ama raia anaheshimu haki hizo.

Aidha, Haki za Binadamu zimeingizwa rasmi katika Katiba ya Jamhuri ya Mungano wa Tanzania. Hata hivyo, baadhi ya wachambuzi wameeleza kwa ufasaha kwamba Katiba imeingiza vifungu hivyo kwa mkono wa kulia na kuviondoa kwa mkono wa kushoto. Maana yake ni kwamba katika Katiba hiyo hiyo zipo ibara zinazomhakikishia kila mtu kulindiwa uhai, heshima na utu wake, lakini katika vifungu hivyo hivyo, au vingine katika katiba hiyo hiyo vinaweka masharti magumu kwa mtu kuweza kufaidi haki hizo

Haki za Binadamu zinatambuliwa ulimwenguni kote. Kilichoisukuma Jumuiya ya Kimataifa kuhakikisha kunakuwa na mifumo thabiti ya Ulinzi wa Haki za Binadamu ni mateso na uhalifu mkubwa dhidi ya binadamu uliofanyika wakati wa vita vya pili vya Dunia vilivyoanza tarehe 1 Septemba, mwaka 1939 na kumalizika tarehe 2 Septemba, mwaka 1945. Ni vita vilivyoshuhudia unyama wa hali ya juu unaoweza kufanywa na mwanadamu dhidi ya mwanadamu mwingine, hususan yule aliye dhaifu kimamlaka, kinguvu, kiuchumi, kisiasa, nk.

Kwa hiyo, mnamo mwaka 1948 mataifa yapatayo 50 chini ya wavuli wa Umoja wa Mataifa yalikutana na kutengeneza orodha ya mambo ambayo yalikuja kufahamaika kama Tamko la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu. Kuanzia wakati huo, kila nchi ikaendelea kuzilinda haki hizo kwa ama kuzitungia sheria, au kuziingiza katika Katiba za nchi zao. Mpaka sasa, Tamko hilo limefasiliwa katika lugha zaidi ya 360 duniani kote.

Hata hivyo, miaka mingi kabla ya vita vya pili vya Dunia vilivyoisukuma jumuiya ya kimataifa kukaa pamoja na kutengeneza tamko la haki za binadamu, tayari katika nchi ya Uingereza na maeneo mengine kulikuwa kumeshafanyika juhudi kadhaa za kutambua, kuheshimu na kulinda haki za binadamu tangu karne ya 13

Kwa ujumla, haki za binadamu ni kitu ambacho kila mtu anapaswa kuwa na ufahamu wa asili wa kujua kama zimevunjwa ama hazijavunjwa. Hata kwa hisia tu. Kwa mfano, katika hali ya kawaida tunatarajia kwamba ukimwona askari polisi anampiga mtuhumiwa badala ya kumfumga pingu na kumpeleka kituoni kwa mahojiano ya kina utafahamu mara moja kwamba jambo hilo si sawa. Vilevile, ukiona mtu amenyimwa ajira kwa sababu tu ya kabila lake, rangi ya ngozi ama sura yake utafahamu kwamba jambo hilo si sawa na linafaa kurekebishwa haraka sana.

Pia, haki za binadamu zinaweza kutumika kama kipimo cha ustaarabu ambacho jami husika imekifikia. Mara nyingi, jamii ambazo hazijastarabika zinaongoza kwa uvunjaji wa haki hizo, bila kujali kama wahusika ni wasomi ama la.

Haki za binadamu zinahusu usawa, heshima, staha, utu na utashi. Kila mtu anayeamini anastahili kuheshimiwa anapaswa pia kuheshimu wengine. Halikadhali, kila mtu anapaswa kulinda uhai na maslahi halali ya watu wengine.

Kutokana na maelezo hapo juu, kila mtu mwenye akili timamu anaweza kujua ni jambo lipi lenye hadhi ya kuitwa Haki za Binadamu. Kwa ufupi ni kwamba namna rahisi ya kujua haki za binadamu ni zipi ni kwa kuangalia yale mambo ambayo mwanadamu anastahili kutendewa kwa sababu tu amezaliwa akiwa binadamu, tofauti na wanyama wengine.

Tukutane toleo lijalo